WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 73 | Disemba 1 - 31 2025



# WAZIRI MKUU APONGEZA TPDC KWA UJENZI WA SHULE YA MSINGI LIKONG'O

WIZARA YA NISHATI   +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**
Dkt. James Mataragio

**MHARIRI MKUU**
Nteghenjwa Mbwambo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Teresia Mhagama

**WAANDISHI**
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Felista Charles
Judith Hasani

**WAPIGA PICHA**
Amanzi Kimonjo
Charles Mushi
Petro Mwanda
Ruben Richard

**MSANIFU KURASA**
Brian Mbaga

© NISHATI 2026


Nishati Safi
ya Kupikia
OKOA MAISHA
NA MAZINGIRA


Nishati Safi
ya Kupikia

# WAZIRI MKUU APONGEZA TPDC KWA UJENZI WA SHULE YA MSINGI LIKONG'O

- Akumbusha shule kufungwa miundombinu ya Nishati Safi ya Kupikia kuunga mkono jitihada za Rais Samia



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Mwigulu Nchemba akipongeza Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa ujenzi wa shule bora ya Awali na Msingi katika Kijiji cha Likong'o

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Mwigulu Nchemba amepongeza Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa ujenzi wa shule bora ya Awali na Msingi katika Kijiji cha Likong'o mkoani Lindi ambako mradi wa uzalishaji na usindikaji wa Gesi Asilia kuwa kimiminika ( LNG) utatekelezwa.

Waziri Mkuu ametoa pongezi hizo tarehe 20 Desemba 2025 wakati akikagua ujenzi wa shule hiyo itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 katika Kijiji cha Likong'o, Kata ya Mbanja, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

"Nawapongeza TPDC kwa hatua hii ya kutekeleza shughuli za uwajibikaji kwa jamii (CSR). Shule hii ni bora, ya kisasa na imezingatia mahitaji mbalimbali ikiwemo kuwa na miundombinu inayokidhi watu wenye mahitaji maalum na watoto wa kike." Amesema Mhe. Nchemba

Katika hatua nyingine Dkt. Nchemba ameelekeza Wizara ya Nishati kuhakikisha kuwa shule hiyo inafungwa miundombinu ya Nishati Safi ya Kupikia kuunga mkono utekelezaji wa Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia ambayo kinara wake ni Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kutokana na uwepo wa shule hiyo, Waziri Mkuu amewaasa wananchi kuchangamkia fursa kwa kuwasomesha watoto wao na hivyo kuunga mkono jitihada anazofanya Rais Rais Samia za ujenzi shule katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwawezesha watoto wote kupata



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Mwigulu Nchemba akikaguwa ujenzi wa shule bora ya Awali na Msingi katika Kijiji cha Likong'o mkoani Lindi.

elimu.

Kwa upande wake Mhe. Salome Makamba ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati, amesema mradi wa ujenzi wa Shule ya Msingi Likong'o unatekelezwa kama sehemu ya kurudisha fadhila kwa wananchi waliotoa ardhi kwa ajili ya utekelezaji mradi wa LNG.

Ameeleza kuwa ujenzi wa Shule hiyo ambao umefikia asilimia 70 unaonesha jinsi kaulimbiu ya kazi na utu inavyotekelezwa kwa vitendo na Serikali ya Awamu ya Sita.

Katika hatua nyingine, Mhe. Salome ameeleza kuwa agizo la Waziri Mkuu la shule hiyo kuwekewa miundombinu ya nishati safi ya kupikia litatekelezwa.

Naye, Mbunge wa Lindi, Mhe. Mohamed Utaly, amemshukuru Rais Samia kwa dhamira ya kuwekeza katika mradi wa LNG ambao amesema utaleta chachu ya elimu mkoani Lindi.

Awali, Mhandisi Msimamizi wa mradi wa shule ya Awali na Msingi Likong'o, Upendo Mahavanu kutoka TPDC alisema mradi huo unagharimu Sh .bilioni 1.27 ambapo shule itakuwa na Madarasa 9; saba yakiwa ni ya shule msingi na mawili ni ya awali. Pia kutakuwa na ofisi na nyumba za walimu.

Utekelezaji wa mradi wa LNG unatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali nchini ikiwemo mapato ya Serikali yatakayotokana na uuzaji wa LNG kwenye soko la kimataifa, fursa za ajira, fursa kwa wazawa kuuza bidhaa, uhaulishaji wa teknolojia mbalimbali ili kuwajengea uwezo wataalam wa ndani n.k



Muonekano wa madarasa katika shule ya Awali na Msingi ya Likong'o mkoani Lindi.

# NDEJEMBI AZINDUA MKAKATI NA MPANGO KAZI WA MAGEUZI YA NISHATI UTAKAOTEKELEZWA NA NCHI ZA AFRIKA

- Ni katika Kongamano la Nishati la AU linalofanyika nchini Ethiopia
- Aeleza umuhimu wa nchi za Afrika kutumia nishati safi ili kutunza mazingira na kupunguza hewa ukaa
- Asema Tanzania inatekeleza lengo la kufikisha umeme kwa wananchi wote ifikapo 2030



Waziri wa nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi akizindua Mkakati na Mpango Kazi wa Mageuzi ya Nishati ambao utatekelezwa na Nchi za Afrika kupitia Kamisheni ya Nishati ya Afrika (AFREC).

Waziri wa nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi amezindua Mkakati na Mpango Kazi wa Mageuzi ya Nishati ambao utatekelezwa na Nchi za Afrika kupitia Kamisheni ya Nishati ya Afrika (AFREC).

Uzinduzi huo umefanyika katika muendelezo wa Kongamano la Nishati la Umoja wa Nchi za Afrika (AU) linalofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia na kushuhudiwa na Mawaziri wa Nishati wa Nchi za Afrika, Washirika wa Maendeleo na Wadau wa Nishati.

Katika uzinduzi huo, Mhe. Ndejembi ameeleza umuhimu wa Nchi za Afrika kutumia Nishati Safi katika kuzalisha umeme viwandani, majumbani, usafiri na majengo ili kutunza mazingira na kupunguza hewa ukaa ambapo kwa Afrika inakadiriwa kufikia asilimia nne.

Katika utekelezaji wa mkakati huo Mhe Ndejembi amezihimiza Nchi za Afrika kutumia vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme ili kuhakikisha kuwa watu milioni 600 barani Afrika wanafikiwa na huduma ya umeme.

" Tukiwa kama Viongozi wa Afrika tuna jukumu la kuhakikisha watu wetu wote wanapata huduma ya umeme ya uhakika. Tayari Tanzania kupitia mpango wa mission 300 tumejiwekea lengo la kuhakikisha ifikapo Mwaka 2030 watanzania wote wanapata huduma ya umeme ambapo hadi sasa tayari tumefikia asilimia 85," Amesema Mhe. Ndejembi.

Katika kongamano hilo, Mhe Ndejembi ameambatana na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga.


Picha ya pamoja katika muendelezo wa Kongamano la Nishati la Umoja wa Nchi za Afrika (AU) lililofanyika Jijini Addis Ababa, Ethiopia na kushuhudiwa na Mawaziri wa Nishati wa Nchi za Afrika, Washirika wa Maendeleo na Wadau wa Nishati.

# NCHI ZA AFRIKA ZAHIMIZWA KUSHIRIKIANA KATIKA KUIMARISHA MATUMIZI BORA YA NISHATI

- Ni katika kutekeleza mikakati na mipango ya kuendeleza matumizi bora ya Nishati Afrika
- Tanzania Yapiga Hatua Kubwa Katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia
- Ushirikiano wa Serikali, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo Wawekewa Mkazo



Picha ya pamoja kwenye Kongamano la Nishati la Umoja wa Nchi za Afrika (AU) lililofanyika Makao Makuu ya Umoja huo "Addis Ababa nchini Ethiopia.

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi ametoa wito kwa Nchi za Afrika kuungana kwa pamoja katika kutekeleza mikakati na mipango ya kuendeleza matumizi bora ya Nishati, ili kuokoa upotevu wa Nishati pamoja na fedha ambazo zingetumika kwa uwekezaji usiohitajika.

Mhe.Ndejembi ametoa wito huo wakati akihutubia Kongamano la Nishati la Umoja wa Nchi za Afrika (AU) katika Makao Makuu ya Umoja huo Addis Ababa nchini Ethiopia.

"Nchi za Afrika zinapokutana hapa kama wadau wa sekta ya Nishati ni lazima tuungane kwa pamoja katika kutekeleza mipango yetu kwa ajili ya Afrika yetu kwani Serikali ya Tanzania ipo tayari kufanya kazi na Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo na Wadau wote katika kuhakikisha tunapiga hatua kubwa ya kiuchumi na kijamii," Amesema Mhe Ndejembi.

Aidha Mhe Waziri Ndejembi ameshiriki mjadala wa Mawaziri wa Nishati wa Nchi za Afrika ambapo alitoa taarifa ya hatua kubwa iliyopigwa na Tanzania katika kusimamia ufanisi wa Nishati pamoja na matumizi ya Nishati safi ya kupikia.

Mhe. Ndejembi ameeleza kuwa Tanzania tayari imeshazindua na kutekeleza mkakati wa Taifa wa miaka 10 wa matumizi ya Nishati safi ya kupikia (2024-2034), sambamba na mkakati wa Mawasiliano na kuandaa mpango kazi wa kutekeleza mikakati hiyo ili kuufikia umma wa Watanzania.

" Nchini Tanzania hadi kufikia Novemba 2025 tayari asilimia 23.2 ya wanachi wanatumia Nishati safi ya kupikia ikilinganishwa na asilimia 6.9 ya mwaka 2021, hivyo kama Taifa tumepiga hatua kubwa na ni matarajio yetu tutaongeza idadi kubwa zaidi ya watumiaji wa nishati safi," Amesema Mhe Ndejembi.

Katika ziara hiyo Mhe Waziri Ndejembi ameambatana na Kamishna wa Umeme na Nishati jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga.



Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi akitoa wito kwa Nchi za Afrika kuungana kwa pamoja katika kutekeleza mikakati na mipango ya kuendeleza matumizi bora ya Nishati.

# NDEJEMBI KUSHIRIKI KONGAMANO LA MAWAZIRI WA NISHATI WA AU NCHINI ETHIOPIA

- Kujadiliana mikakati ya kuendeleza matumizi bora ya Nishati
- Mkakati na Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati barani Afrika kuzinduliwa



Kwenye picha ni viongozi mbalimbali wameambatana na Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi Jijini Addis Ababa, Ethiopia kwa ajili ya kushiriki Kongamano la Mawaziri wa Sekta ya Nishati wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) wenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kuendeleza matumizi bora ya nishati kwa Bara la Afrika.

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi amewasili jijini Addis Ababa, Ethiopia kwa ajili ya kushiriki Kongamano la Mawaziri wa Sekta ya Nishati wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) wenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kuendeleza matumizi bora ya nishati kwa Bara la Afrika.

Kongamano hilo litafanyika kwa siku mbili ambapo nchi wanachama wa AU watabadilishana uzoefu katika mikakati, mipango, changamoto na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza ya miradi ya kuongeza ufanisi wa nishati katika bara la Afrika

Katika kongamano hilo pia Mkakati na Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati barani Afrika utazinduliwa ambao unaendana na malengo ya Mpango wa Afrika wa Mwaka 1963.

Aidha kongamano hilo la siku mbili limetanguliwa na mafunzo kwa wataalamu wa sekta ya Nishati katika kuwajengea uzoefu kwenye maeneo ya kupunguza Matumizi ya umeme katika sekta za majengo, viwanda, usafiri pamoja na majumbani.

Katika kongamano hilo Waziri Ndejembi ameongozana na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga.

Nchini Ethiopia Waziri Ndejembi amepokelewa na Balozi na Mwakilishi wa Kudumu wa Umoja wa Afrika (AU) na Kamisheni ya Uchumi Afrika (UNECA), Mhe. Innocent Shiyo.

# BARAZA LA WAFANYAKAZI WIZARA YA NISHATI LAJENGEWA UELEWA KUHUSU DIRA 2050

- Nishati ni moja ya vichocheo vya Dira 2050
- Waelimishwa pia kuhusu mafao ya PSSSF na usalama wa kifedha


Kwenye picha ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu Bi. Ziana Mlawa akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati Mkoani Morogoro.

Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wamejengewa uelewa kuhusu mwelekeo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya taifa kuelekea maendeleo ya muda mrefu na endelevu.

Akizungumza Mkoani Morogoro, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kutoka Tume ya Taifa ya Mipango, Bw. Titus Kaguo, amesema kuwa kufuatia kukamilika kwa Dira ya 2025, taifa linaelekea katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050, ambayo inalenga kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2035 na uchumi wa kipato cha juu ifikapo mwaka 2050.

"Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Tanzania Development Vision 2025) ilikuwa mpango wa maendeleo wa muda mrefu wa miaka 25 ulioliongoza taifa katika kufikia uchumi wa kipato cha kati na kuweka msingi wa maendeleo ya kisasa.Dira hiyo ilijikita katika sekta muhimu ikiwemo nishati, kilimo, viwanda, miundombinu na teknolojia, ambazo zimekuwa nguzo kuu za maendeleo ya taifa." Amesema Kaguo

Ametaja vichocheo vya Dira 2050 kuwa ni nishati, usafirishaji fungamanishi, sayansi na teknolojia, utafiti na maendeleo pamoja na mageuzi ya kidijitali

Aidha, wajumbe hao pia walipatiwa elimu kuhusu mafao yanayotolewa na Mfuko wa Pensheni, Akiba na Hifadhi ya Jamii (PSSSF), ambayo ni nguzo muhimu ya ustawi wa watumishi wa umma.

Mafao hayo ni pamoja na pensheni ya uzeeni, mafao ya ulemavu, ajali, uzazi, ugonjwa, mafao ya wafiwa pamoja na msaada wa mazishi. Kupitia mafao hayo, watumishi wa umma na familia zao hupata usalama wa kifedha katika nyakati za dharura na kipindi cha baada ya kustaafu, hatua inayochangia kuboresha maisha na kuimarisha uhakika wa mustakabali wa kifedha.


Kwenye picha ni wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wakijengewa uelewa kuhusu mwelekeo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya taifa kuelekea maendeleo ya muda mrefu na endelevu.

# WANANCHI KUNUFAIKA NA HUDUMA ZA KIJAMII MRADI WA LNG MKOANI LINDI

- Ndejembi asisitiza TPDC kutanguliza uzalendo katika utekelezaji wa mradi



Waziri Ndejembi akieleza namna utekelezaji wa mradi wa kubadilisha gesi asilia kuwa kimiminika ( LNG) unavyotarajiwa kuwanufaisha wazawa kwa kiasi cha takribani dola za Marekani milioni 10 (USD 10M).

Waziri Ndejembi ameeleza kuwa utekelezaji wa mradi wa kubadilisha gesi asilia kuwa kimiminika ( LNG) unatarajiwa kuwanufaisha wazawa kwa kiasi cha takribani dola za Marekani milioni 10 (USD 10M) pindi mradi huo utakapoanza kupitia shughuli za uwajibikaji kwa jamii (CSR), pamoja na kuliingizia taifa mapato mbalimbali yakiwemo kodi za zuio na kodi ya mapato ya kampuni.

Akizungumza katika kikao na Watendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kilichofanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma, Waziri Ndejembi amesema kuwa mradi huo utakaotekelezwa katika kijiji cha Likong'o mkoani Lindi ni wa kimkakati kwa maendeleo ya taifa, hivyo ni muhimu kufuata taratibu na miongozo iliyopo ili kuhakikisha Watanzania wananufaika kikamilifu na rasilimali hiyo.

Ameongeza kuwa Halmashauri zitafaidika moja kwa moja kupitia miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika maeneo husika.

Ndejembi amesema mradi huo utafungua fursa kwa sekta nyingine za uzalishaji ikiwemo sekta ya madini na sekta nyingine muhimu, hatua itakayochochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

Katika kikao hicho amesisitiza umuhimu wa kutoa elimu kwa Watanzania mapema kuhusu mradi huo wa gesi asilia na faida zake ili kujenga uelewa na uungwaji mkono wa wananchi.

Kwa upande mwingine Mhe. Ndejembi, amewataka wataalamu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuzingatia uzalendo na kutanguliza maslahi mapana ya taifa katika utekelezaji wa mradi wa kuchakata gesi asilia kuwa kimiminika ( LNG).



Picha ya pamoja kwenye kikao alichohudhuria Waziri wa nishati Mhe. Ndejembi na Watendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kilichofanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma,

# MAADILI KAZINI YAWE MSINGI WA UTOAJI HUDUMA KWA WANANCHI – NDEJEMBI

- Awataka Watumishi Sekta ya Nishati kujiepusha na rushwa, ubadhirifu na uzembe
- Asisitiza uzalishaji wa umeme kwa vyanzo mchanganyiko
- Lengo ni kufikisha megawati 8,000 ifikapo 2030
- Ataka Elimu ya Nishati Safi ya Kupikia kuwa endelevu




Picha ya pamoja ya Viongozi mbalimbali waliposhiriki mkutano wa Baraza la Wafanyakazi Mkoani Morogoro.

Watumishi katika Wizara ya Nishati wametakiwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili kuendelea kutoa huduma bora kwa Watanzania, hususan kwa kujiepusha na vitendo vya rushwa, ubadhirifu na uzembe mahali pa kazi.

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratias Ndejembi ameyasema hayo wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati uliofanyika mkoani Morogoro.

Akizungumza katika mkutano huo, Mhe. Ndejembi amesema maadili ya kazi ni nguzo muhimu katika kukuza sekta ya nishati na kuharakisha maendeleo ya Taifa, akibainisha kuwa nishati ikiwemo umeme, mafuta na gesi ni mhimili mkubwa wa uchumi wa nchi.

"Zingatieni maadili kazini katika utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kujiepusha na vitendo vya rushwa, ubadhirifu na uzembe mahali pa kazi, ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za umeme, mafuta na gesi," amesema Mhe. Ndejembi

Aidha, amewataka watumishi wa Wizara kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na weledi ili kuendelea kuchochea maendeleo ya sekta ya nishati na kukuza uchumi wa Taifa.

Kuhusu upatikanaji wa umeme wa uhakika, amesema Wizara ya Nishati ina jukumu la kuhakikisha Tanzania inazalisha jumla ya megawati 8,000 za umeme ifikapo mwaka 2030 kupitia vyanzo mchanganyiko, ikiwemo utekelezaji wa miradi mipya ya uzalishaji umeme.

Ameongeza kuwa katika kufikia lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuweka vipaumbele sahihi vya nishati ili kuhakikisha miradi ya kimkakati inatekelezwa kwa wakati.

Vilevile, amewataka watendaji wa Wizara kupitia Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia kuendelea kutoa elimu ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi ili kufikia lengo la asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034, kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme, gesi na mafuta ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za nishati zilizo bora, salama na za uhakika.

# MRADI WA USAMBAZAJI UMEME VITONGOJINI SIHA-KILIMANJARO WAZINDULIWA

- Lengo la mradi ni kuunganishia umeme kaya 5,000 ifikapo 2030
- Kaya 3000 tayari zimefaidika na mradi
- Mhe. Salome asema dhamira ya Rais Samia ni kuiangaza Tanzania nzima kwa nishati ya umeme
- Asema mpango wa Misheni 300 unatekelezwa kwa kasi Tanzania


Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba akizindua mradi wa usambazaji wa umeme katika vitongoji vya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba amezindua mradi wa usambazaji wa umeme katika vitongoji vya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, akisisitiza kuwa Serikali itaendelea kutekeleza dhamira ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa na huduma ya nishati ya umeme.

Akizungumza wilayani Siha, wakati wa hafla ya uzinduzi, Mhe. Makamba amesema kuwa pamoja na umeme kuunganishwa kwenye kaya, Wizara ya Nishati inaendelea kuhakikisha taasisi za umma, hususan shule, zinaunganishwa pia na umeme ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Katika hafla hiyo, Naibu Waziri aliwasha rasmi umeme katika Kitongoji cha Ngare-Nairobi na kueleza kuwa, "tumeanza na kitongoji hiki lakini katika Wilaya ya Siha pekee Serikali inatekeleza mpango wa kuwasha umeme kwa kaya 5,000 ifikapo mwaka 2030. Hadi sasa kaya 3,000 tayari zimeunganishwa na umeme."

Katika hatua nyingine, Mhe. Salome amesema Tanzania inaendelea kutekeleza kwa kasi Mpango Mahsusi wa kuwafikishia umeme Waafrika Milioni 300 ifikapo mwaka 2030 (Mission 300) ukiwa na lengo la kuhakikisha wananchi wote nchini wanafikiwa na huduma ya umeme ifikapo mwaka 2030.

"Kupitia Mpango wa Misheni 300, TANESCO inalenga kuunganishia umeme wananchi 1,700,000 kwa mwaka ambapo Mkoa wa Kilimanjaro pekee unalenga kuunganisha wananchi 12,000 kwa mwaka na hadi sasa zaidi ya wananchi 9,000 tayari wamepata huduma ya umeme mkoani humu." Amesema

Kwa upande wake, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Kilimanjaro, Mha. Merry Kabakuzi amesema Wilaya ya Siha ina jumla ya vitongoji 169 ambapo vitongoji 155 tayari vina umeme huku vitongoji 14 vilivyosalia vikiwa katika Mpango wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) awamu ya pili ya ujazilizi wa vitongoji.

Ameeleza kuwa maeneo ambayo umeme umefika kwa kiwango kidogo yataendelea kuongezewa mtandao kupitia Mpango Mahsusi wa misheni 300.

# TPDC NA PURA HAKIKISHENI WATANZANIA WANANUFAIKA NA RASILIMALI ZA MAFUTA NA GESI - MHE. SALOME

- Awekea mkazo upatikanaji wa ajira, huduma za kijamii na nishati nafuu
- Apongeza PURA na TPDC kwa jitihada wanazofanya katika utafiti na uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia
- Asisitiza mazingira rafiki ya uwekezaji




Picha ya pamoja ya viongozi mbalimbali mara baada ya kikao Jijini Dar es Salaam, na Menejim pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba amefanya ziara katika Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kwa lengo la kuzungumza na Watendaji taasisi hizo mara baada ya kuteuliwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nyadhifa hiyo ambapo amewataka watendaji kuhakikisha Watanzania wananufaika moja kwa moja na uwepo wa rasilimali za mafuta na gesi.

Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Mhe. Salome ameweka mkazo kuhusu upatikanaji wa ajira kwa Watanzania, huduma za kijamii na upatikanaji wa nishati kwa gharama nafuu.

Mhe. Salome pia ameielekeza Menejimenti ya TPDC kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia majumbani ili Watanzania waendelee kunufaika zaidi na rasilimali hiyo muhimu.

Vilevile ameipongeza TPDC kwa jitihada wanazoendelea kufanya katika utafutaji na uendelezaji wa rasilimali za mafuta na gesi asilia nchini kwani uboreshaji huo umeanza kuleta matokeo chanya katika upatikanaji wa nishati hiyo katika maeneo mbalimbali nchini huku akiwataka kuhakikisha jitihada hizo zinawanufaisha wananchi wengi zaidi.

Katika hatua nyingine, Mhe. Salome amewapongeza PURA kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuhakikisha sekta ya mafuta inakua nchini huku akiwahimiza kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki kwa wawekezaji wapya ili kuongeza ajira na kuhakikisha wananchi wanapata manufaa ya moja kwa moja kutokana na rasilimali na uwekezaji uliopo nchini.

Aidha, amesisitiza kuwa miradi ya utafiti na uendelezaji wa gesi asilia, ikiwemo mradi wa LNG, ipewe kipaumbele ili kuongeza tija



Kwenye picha ni Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba alipoongoza kikao na Menejimenti ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kwa lengo la kuzungumza na Watendaji taasisi hizo mara baada ya kuteuliwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

katika uwekezaji na kuhakikisha nchi inanufaika kikamilifu na rasilimali zake huku akisisitiza kuwa taasisi zote zilizo chini ya Wizara lazima ziweke mbele maslahi ya wananchi wakati wa kusimamia miradi ya kimkakati ya nishati lakini pia kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Serikali kuhusu usimamizi, matumizi na faida za rasilimali za gesi asilia.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amewasisitiza TPDC kuongeza kasi ya uzalishaji na upatikanaji wa gesi ili nishati hiyo iwe ya kutosha na inawafikia wananchi huku akiisisitiza PURA kuhakikisha wanawapa wawekezaji kipaumbele katika kuwekeza katika fursa za mafuta na gesi kwa lengo la kuhakikisha Serikali inapata mapato na wananchi wananufaika na miradi hiyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC Mussa Makame amesema shirika linaendelea kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi na kusafirisha nishati ya mafuta na gesi, huku likiandaa vizuri upande wa maboresho ya masoko ili kuongeza ufanisi na upatikanaji wa bidhaa hizo nchini na kueleza kuwa kampuni ipo kwenye hatua za kufanya upanuzi wa miradi ya gesi, ikiwemo utekelezaji wa miradi midogo ya LNG itakayowezesha kusafirisha gesi hiyo katika mikoa mbalimbali kwa gharama nafuu na kwa wakati.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Eng. Charles Sangweni amesema PURA itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi huku ikichangia kufanikisha malengo ya sekta kwa mujibu wa Dira ya Taifa 2050.

# TUNAENDELEA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA UMEME ILI WANANCHI MPATE UMEME WA UHAKIKA - MHE.SALOME

- Kituo cha kuzalisha umeme wa gesi Kinyerezi kuboresha upatikanaji umeme Gongo la Mboto na Mbagala
- Amshukuru Dkt. Samia kwa uwekezaji mkubwa sekta ya umeme
- Apongeza mitambo ya umeme kuendeshwa na wazawa.



Kwenye picha ni Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba wakati wa ziara yake ya kukagua Vituo vya kufua umeme kwa njia ya gesi vya Kinyerezi na Ubungo.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba, amesema kuwa Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha miundombinu ya umeme nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika.

Mhe. Salome ameyasema hayo Jijini Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya kukagua Vituo vya kufua umeme kwa njia ya gesi vya Kinyerezi na Ubungo.

Aidha, ameeleza kuwa Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya umeme nchini kwa kutekeleza miradi mipya ya kuzalisha umeme kupitia gesi asilia ili kuongeza upatikanaji wa nishati hiyo kwa wananchi.

Amesema Kituo cha kuzalisha umeme kwa gesi katika kituo cha Kinyerezi utakuwa na mchango mkubwa kwa wakazi wa Gongo la Mboto na Mbagala, ambao wamekuwa wakitegemea umeme kwa shughuli za viwanda na biashara.

"Uzalishaji wa umeme kwa njia ya gesi Kinyerezi utayapa maeneo ya Mbagala na Gongo la Mboto umeme wa uhakika kwani maeneo haya yana watu wengi na viwanda vingi hatahivyo mpaka sasa transfoma ya MVA 120 imeshafungwa na majaribio yameanza hivyo itaboresha upatikanaji wa umeme majumbani na viwandani kwa wananchi wa maeneo hayo. Amesema Mhe. Salome

Mhe. Salome amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza katika Sekta ya umeme kwani utekelezaji wa miradi hiyo yote ya umeme inalenga kuhakikisha Watanzania wanapata nishati bora, ya uhakika na yenye kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, amelipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya umeme lakini pia kwa kuhakikisha waendesha mitambo hiyo ni wazawa hivyo kuongeza ujuzi wa ndani na kupunguza gharama za uendeshaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Bw. Lazaro Twange ameeleza kuwa miradi hiyo ina manufaa makubwa kwa wakazi wa Dar es Salaam, kwani inaboresha uwezo wa miundombinu kuendana na ongezeko la mahitaji ya kila siku huku akisisitiza kuwa kutokana na uzalishaji wa umeme katika kituo cha Kinyerezi wananchi wameendelea kupata umeme wa uhakika na wakudumu katika matumizi ya majumbani na viwandani.

# WAZIRI NDEJEMBI ATAKA HAKI NA USAWA KUZINGATIWA KWA WAWEKEZAJI WA MAFUTA.

- Lengo ni Kulinda maslahi ya Taifa na kuweka Mazingira Bora kwa Wawekezaji
- Ameeleza kuwa EWURA ni Taasisi Muhimu kwa usalama wa Nchi.
- Asisitiza uwepo wa Akiba ya Mafuta kwa ajili ya dharura.



Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi pamoja na viongozi wengine walipotembelea na kufanya kikao na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Waziri wa Nishati, Mhe. Deugratius Ndejembi, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuhakikisha inatenda haki kwa wawekezaji katika sekta ya mafuta bila upendeleo wowote, na kusisitiza kuwa maamuzi yote yafanywe kwa kuzingatia sheria, taratibu na haki, na siyo kwa kuangalia majina au watu binafsi, ili kulinda mazingira bora ya uwekezaji nchini.

Mhe. Ndejembi ametoa maagizo hayo Jijini Dodoma wakati akizungumza na Viongozi na Watendaji wa EWURA lengo likiwa ni kujitambulisha na kuona shughuli wanazozifanya.

"Kuna baadhi ya watendaji wa EWURA hutumia madaraka vibaya kwa kuwaonea wawekezaji,



wa vituo vya mafuta kwa kuvifunga na baadhi ya vituo vingine vyenye changamoto kama hiyo kuachwa, hivyo nasisitiza hali hii isiwepo kwani nikibaini uonevu huo hatua za kinidhamu zitachukuliwa hivyo tuzingatie haki na usawa katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa maslahi ya Taifa letu.

EWURA ni Taasisi Muhimu kwa usalama wa Nchi yetu hivyo tuhakikishe tunaweka maslahi ya Taifa mbele ili kuboresha ustawi wa Watanzania sambamba na kukuza uchumi wa nchi yetu huku tukihakikisha tunaweka akiba ya mafuta kwa ajili ya kukabiliana na dharura". Amesisitiza Mhe. Ndejembi.

Aidha Mhe. Ndejembi amesisitiza umuhimu wa uwajibikaji na uadilifu kwa watumishi wa EWURA na kwamba hatomvumilia mtumishi yeyote ambaye atakwenda kinyume na sheria, taratibu na kanuni za kiutumishi .

Kwa upande wake Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mhandisi Innocent Luoga ameipongeza menejimenti ya EWURA kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha sekta ya mafuta inaendelea kukua huku akieleza kuwa Wizara ya Nishati inaendelea kushirikiana na Taasiai zake kuhakikisha maelekezo na vipaumbele vya Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan vinatekelezwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Dkt. James Andilile ameeleza kuwa EWURA imeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari (LPG) pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa mafuta maeneo ya Vijijini.

# PBPA HAKIKISHENI WAWEKEZAJI WAZAWA WANAPEWA KIPAUMBELE KATIKA FURSA ZA UWEKEZAJI - MHE.SALOME

- Lengo ni kujenga uchumi wa endelevu unaowanufaisha Watanzania wengi zaidi
- Aitaka PBPA kuhakisha mafanikio yanayofanywa na Serikali kupitia taasisi hiyo kujulikana kwa Umma



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba, akitoa wito kwa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kuhakikisha wanatoa fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wazawa ili kuongeza ushindani na kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika sekta ya nishati.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba, ametoa wito kwa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kuhakikisha wanatoa fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wazawa ili kuongeza ushindani na kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika sekta ya nishati.

Mhe. Salome ametoa wito huo Jijini Dar es Salaam katika ofisi za PBPA, wakati wa ziara yake ya kuzungumza na viongozi wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati.

Amesema kuwa ni muhimu PBPA kuweka mazingira rafiki yatakayowezesha makampuni ya ndani kushiriki kikamilifu katika shughuli za uagizaji, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta.

“ Taarifa kama hii ya uwepo wa makampuni yanayouza mafuta takribani 86 ambapo makampuni ya nje ni matano tuu inapaswa kujulikana na umma wa watanzania ili dhamira ya serikali ya awamu ya sita kuwawezesha wazawa ijulikane ili watanzania kuona wazawa wanapewa nafasi ya kushiriki kikamilifu katika uwekezaji huu ili tuweze kujenga uchumi endelevu unaowanufaisha Watanzania wengi zaidi,”Amesisitiza Mhe. Salome.

Sambamba na hilo Mhe. Salome



Picha ya pamoja ya viongozi mbalimbali waliombana na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba alipotembelea Wakala wa Uagizaji Mafuta (PBPA) Jijini Dar es salaam.

ameeleza kuwa ni muhimu kufanya kazi kwa karibu na wafanyabiashara wanaofanya kazi na Taasisi ili kujiimarisha zaidi kiuchumi lakini pia ameelekeza PBPA kuhakikisha wanafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara nyingine kwa lengo la kujiimarisha zaidi.

Katika hatua nyingine Mhe. Salome ameeleza kuwa katika kuelezea mafanikio yanayofanywa na taasisi hiyo ni muhimu kazi nzuri inayotekelezwa kuonekana na kueleweka kwa umma kupitia mbinu za kisasa za Mawasiliano huku akisisitiza kuwa katika dunia ya sasa, wananchi wanahitaji taarifa sahihi, za haraka na zinazoeleweka kirahisi ili kutambua thamani ya kazi inayofanywa na serikali pamoja na taasisi zake.

"Niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoifanya lakini ili kazi hii ionekane lazima tutumie Mawasiliano ya kisasa ambayo yanafikia watu wengi kwa uwazi na kwa wakati," amesema Mhe. Salome.

Ameongeza kuwa matumizi sahihi ya kutoa taarifa zinazofanywa na Taasisi kwa kuwasilisha ujumbe muhimu kwa wananchi zinaweza kuimarisha mahusiano na jamii, kuongeza uwajibikaji na kuhakikisha kila mwananchi anaona matokeo ya kazi inayofanywa kwa manufaa ya Taifa.


Awali akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa kuagiza mafuta kwa pamoja( PBPA) Bw. Erasto Simon ameeleza kuwa PBPA imeendelea kujiimarisha zaidi katika kuhakikisha mifumo inaboreshwa mara kwa mara lakini pia kuendelea kujifunza kutoka kwa wengine

"Sisi kama PBPA tumeendelea kujiimarisha zaidi katika miundombinu ya mafuta kwani toka tumeanza 2019 mpaka sasa 2025 tumehakikisha nchi inakua na mafuta ya kutosha lakini pia nchi nyingine ikiwemo Zimbabwe Malawi na Msumbiji zimeendelea kuja kujifunza kutoka kwetu hivyo hii ni hatua kubwa zaidi inayoonesha mafanikio katika sekta hii.

Aidha ameeleza kuwa kqtika kuboresha utendaji kazi, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya (Single Receiving Terminal) hatua inayolenga kuongeza ufanisi wa upokeaji bidhaa za mafuta na kuimarisha ushindani hivyo mradi huu ukikamilika unatarajiwa kupunguza msongamano wa shehena, kuongeza kasi ya huduma na kurahisisha shughuli za kupakia na kupakua mafuta.

# UWEKEZAJI MKUBWA ULIOFANYWA NA SERIKALI KITUO CHA GESI ASILIA MLIMANI WALETA NAFUU KWA WANANCHI

- Kituo kina uwezo wa kujaza gesi asilia kwenye magari na bajaji 800 kwa siku
- Mhe. Salome Makamba ahamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika eneo la gesi asilia
- Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro na Tanga kufikiwa na vituo vya gesi asilia


Kwenye picha ni Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati wakiwa pamoja na uongozi wa Gereza Urambo Mahabusu kwenye ziara ya kuangalia namna agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia lilivyotekelezwa.

Naibu waziri wa Nishati Mhe.Salome Makamba ameeleza kuwa, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika kujenga kituo cha kujaza gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri katika eneo la Mlimani jijini Dar es Salaam ambapo zaidi ya sh.Bilioni 12 zimetumika kukamilisha kituo hicho chenye uwezo wa kuhudumia magari madogo na bajaji 800 kwa siku.

Mhe.Salome amebainisha hayo Jijini Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya kukagua kituo hicho kinachosimamiwa na Kampuni Tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania(TPDC) ya GASCO.

Mhe. Salome ameeleza kuwa Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inahakikisha rasilimali zilizopo zinawanufaisha wananchi kwa namna mbalimbali.

"Matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) yamerahisisha gharama za maisha kwa watu wa vyombo vya usafiri kwani gharama ya gesi kilo moja ni shilingi 1500 ambapo ukiwa na mtungi wa Kilo 17 unaweza kusafiri umbali wa KM 50 hii inaonesha dhahiri kuwa gesi inagharama nafuu zaidi kuliko mafuta lakini pia kutokana na wingi wa magari ya biashara na bajaji katika mkoa wa Dar es Salaam uwekezaji huu umekuwa ni fursa kwa wafanyabiashara hao katika kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza kipato." Amesema Mhe. Salome

Ameeleza kuwa, hadi kufikia Juni 2026 kutakuwa na vituo vingine vya kujaza gesi katika maeneo ya kila barabara kubwa ya Mkoa wa Dar es Salaam huku akisiaitiza kuwa Serikali pia imeanza mpango wa kujenga vituo vikubwa katika



Kwenye picha ni Naibu waziri wa Nishati Mhe.Salome Makamba ameambatana na viongozi mbalimbali katika ukaguzi wa kituo cha kujaza gesi kinachosimamiwa na Kampuni Tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania(TPDC) yani GASCO.

Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro na Tanga ambavyo vitasaidia wananchi wa mikoa hiyo kupata huduma lakini pia wananchi wa Mikoa ya karibu kunufaika na huduma husika.

Mhe.Salome ametoa wito kwa sekta binafsi kuongeza kasi ya uwekezaji katika miundombinu ya gesi asilia, akibainisha kuwa mahitaji ya nishati nafuu yanaongezeka kwa haraka nchini hivyo ni fursa kwao kuwekeza ili kurahisisha upatikanaji wa nishati hiyo kwani Serikali imeboresha mazingira ya uwekezaji kupitia mfumo wa ushirikishwaji wa Biashara kati ya Serikali na sekta binafsi (PPP) hasa kupitia mfumo wa One Stop Centre ambao ni rahisi kufikisha huduma kwa wananchi.

Sambamba na hilo amesisitiza kuwa Serikali inaendelea kutoa kipaumbele kwa vijana kwani sekta ya gesi na mafuta inawagusa moja kwa moja vijana wanaofanya biashara za bolt na bajaji kwani gharama za uendeshaji ni nafuu zaidi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Bw. Mussa Makame ameeleza kuwa kituo cha kujaza gesi Mlimani kina uwezo wa kujaza hadi kilogrmu elfu 70 lakini kwa sasa kinajaza hadi kilogramu 50 kwa bajaji, magari madogo pamoja na magari makubwa.

"Zamani kabla ya kujengwa kwa kituo hiki cha Serikali wananchi walikuwa wakijaza gesi katika vituo binafsi ambapo walikuwa wakitumia masaa matatu lakini kwa sasa gari zinatumia dakika nne kujaza gesi na kwa siku kinajaza magari madogo na bajaji 800 lakini magari makubwa 15 yanayopeleka gesi katika vituovidogo.

Amesema kwa kushirikiana na Sekta binafsi Serikali itahakikisha kufikia 2026 Dar es Salaam inakuwa na vituo vikubwa 15 vya kujaza gesi lakini pia Mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Nao wanufaika wa gesi asilia wameishukuru Serikali kwa kuanzisha mradi huo pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu kwani mwanzoni walikuwa wakitumia muda mrefu kujaza gesi lakini kwa sasa wanajaza na kuondoka kwa wakati hali inayowasaidia katika kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza kipato.

# TUZINGATIE MATUMIZI YA RASILIMALI ZETU KATIKA KUTEKELEZA MPANGO WA KUZALISHA UMEME WA NYUKLIA NCHINI. PROF. NAJAT.

- Lengo ni kuhakikisha Mpango huu unatekelezwa na Wataalamu wazawa
- Wananchi watakiwa kushirikishwa katika Mpango huo
- Ni Mwelekeo wa Serikali katika Kukidhi Mahitaji ya Umeme Ifikapo 2030



Mkurugenzi Mkuu Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) Prof. Najat Mohammed akifungua kikao cha Kwanza cha Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa kuzalisha umeme kwa kutumia Nishati ya Nyuklia (NEPIO)

Mkurugenzi Mkuu Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania(TAEC) Prof. Najat Mohammed amewataka wajumbe wa Kamati tendaji ya uratibu Mpango wa uzalishaji umeme wa Nyuklia Nchini(NEPIO) kuhakikisha wanaanza maandalizi mapema ya namna mpango huo utakavyotekelezwa Nchini huku akiwasisitiza kuhakikisha wanazingatia matumizi ya rasilimali zinazopatikana Nchini Tanzania katika utekelezaji wa mpango huo.

Hayo ameyabainisha wakati akifungua kikao cha Kwanza cha Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa kuzalisha umeme kwa kutumia Nishati ya Nyuklia (NEPIO) kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Nishati, Mtumba Jijini Dodoma.

Akifungua kikao hicho Prof. Najat Mohammed ameitaka kamati hiyo kuhakikisha wanaanza maandalizi mapema ili kukamilisha mpango huu ndani ya miaka saba
"Matayarisho ya Mpango huu yanachukua miaka 10 lakini sisi tunataka tuende miaka saba ili kupata umeme huu kwa muda mfupi zaidi hivyo niwatake muanze maandalizi mapema ili mfanye utafiti wa rasilimali zitakazotumika ili kama rasilimali hizo zinapatikana hapa nchini zitumike rasilimali zetu."Amesisitiza Prof. Najat.

Amesema kuwa kuwepo na mnyororo wa ugavi(supply chain) thabiti na endelevu katika mpango wa kuzalisha umeme wa nyuklia nchini kwa kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi, na wadau wa kimataifa.

“Katika kutekeleza Mpango huu tuhakikishe upatikanaji wa vifaa, teknolojia, na malighafi muhimu kwa wakati unaofaa, pamoja na kujenga uwezo wa ndani wataalamu kupitia mafunzo mbalimbali lakini pia kuhakikisha tunapoalikwa kushiriki mikutano na warsha mbalimbali za masuala ya Nyuklia tunashiriki kikamilifu ili kujifunza zaidi”. Amesisitiza Prof. Mohammed.

Aidha, ameitaka Kamati hiyo kuhakikisha wananchi wanashirikiahwa katika mpango huu ili kuzingatia mifumo madhubuti ya usimamizi wa hatari, viwango vya usalama, na sera rafiki za kisheria kwani wananchi wakishirikishwa na kupewa elimu mpango huu utatekekezwa kwa ufanisi, gharama nafuu na kwa kuzingatia ulinzi wa mazingira pamoja na maendeleo endelevu ya kiuchumi.

Awali akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Mpango wa Nishati ya Nyuklia(NEPIO) Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Wizara ya Mishati Mha. Innocent Luoga ameeleza kuwa kulingana na taratibu za Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu(IAEA) ambapo Tanzania ni mwananchama Nchi zinazotarajiwa kuzalisha umeme wa nyuklia ni lazima kuwa na kamati hiyo hivyo Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na TAEC pamoja na Wizara ya Maji, Nishati na Madini - Zanzibar, TANESCO, ZECO, EWURA, NEMC na ZURA zimekua zikishiriki katika maandalizi ya mpango huu kwa kuzingatia uzoefu na umuhimu wa Taasisi hizo katika kutekeleza mpango huo.



Kwenye picha ni Kamishna wa umeme na nishati Jadidifu Mha. Innocent Luoga aliposhiriki kikao cha Kwanza cha Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa kuzalisha umeme kwa kutumia Nishati ya Nyuklia (NEPIO)

“ Nishati ya Umeme ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na dunia kwa ujumla hivyo kutokana na ongezeko la shughuli za kiuchumi na maendeleo mengine mahitaji ya umeme yanakadiriwa kufikiwa Megawati elfu 8,000 ifikapo mwaka 2030 kutoka Megawati 4,352.13 za sasa hivyo kutokana na ongezeko Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alielekeza kuhakikisha azma hii inatekelezwa ili kuhakikisha tunakua na umeme wa kutosha na kuondokana na mgao wa umeme.”Ameeleza Mha. Luoga.



Mkurugenzi Mkuu Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) Prof. Najat Mohammed akifungua kikao cha Kwanza cha Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa kuzalisha umeme kwa kutumia Nishati ya Nyuklia (NEPIO)

# MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YAFUNGUA FURSA MPYA ZA AJIRA KWA WATANZANIA

- Ni Kupitia uzalishaji wa mkaa mbadala na teknolojia rafiki kwa mazingira
- Wadau wahimizwa kushirikiana na TBS kutengeneza bidhaa zinazokidhi viwango




Kwenye picha ni Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Nolasco Mlay wakati wa ziara yake ya kutembelea Taasisi ya Wazalendo Movement inayojishughulisha na utengenezaji wa mashine za kuzalisha mkaa mbadala pamoja na uzalishaji wa mkaa huo wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Imeelezwa kuwa matumizi ya nishati safi ya kupikia yameendelea kufungua fursa nyingi za ajira kwa Watanzania, hususani katika uzalishaji wa mkaa mbadala na utengenezaji wa mashine za kuzalishia mkaa huo.

Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Nolasco Mlay amesema hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea Taasisi ya Wazalendo Movement inayojishughulisha na utengenezaji wa mashine za kuzalisha mkaa mbadala pamoja na uzalishaji wa mkaa huo wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Bw. Mlay amesema kuwa taasisi nyingi zinazohudumia watu kuanzia 100 na kuendelea zimeanza kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia, jambo linaloongeza kwa kiasi kikubwa mahitaji ya mkaa mbadala na hivyo kuhitaji uzalishaji wa kasi zaidi.

"Niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuzalisha mkaa mbadala pamoja na mitambo ya kutengenezea mkaa huo. Hii ni fursa kubwa kwa Watanzania kwani mahitaji ni makubwa, lakini ni muhimu kuhakikisha mkaa huu unaozalishwa ni wa ubora wa hali ya juu na unaodumu hata ukisafirishwa kwa umbali mrefu," amesisitiza Bw. Mlay

Kwa upande wake, Mhandisi Mwandamizi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Deusdedit Malulu amesisitiza umuhimu wa kushirikisha Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika utengenezaji wa mkaa mbadala ili kuhakikisha bidhaa zinakidhi viwango vinavyotakiwa.

Aidha, amewahimiza wazalishaji kujisajili kwenye mfumo wa NEST



Picha ya pamoja ya Wataalamu kutoka Wizara ya nishati na Wadau kutoka Taasisi ya Wazalendo Movement wakitazama namna uchomaji wa nyama unavyofanyika Mkoani Pwani,

ili kupata fursa mbalimbali na kubainisha kuwa REA ina mpango wa kutoa fursa kwa wananchi katika utengenezaji wa mashine kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa vifaa vya kuzalisha mkaa mbadala.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wazalendo Movement,Bw. Saidi Malema amesema kuwa taasisi hiyo, katika kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, imeanzisha kikundi cha nishati safi ya kupikia kinachojihusisha na uzalishaji wa mkaa mbadala unaotengenezwa kutokana na magunzi ya mahindi na nyasi kavu.

Amesema taasisi hiyo hutengeneza mashine za kuzalishia mkaa zinazotumia umeme na zisizotumia umeme.

Ameongeza kuwa taasisi hiyo pia imeanzisha kikundi cha Nishati Safi Sanaa Group, kinacholenga kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia sanaa ya maigizo na nyimbo.

Amesema Taasisi ya Wazalendo Movement imefanikiwa kuuza mashine zake kwa wadau katika mikoa ya Tabora, Singida na Pwani. Aidha, imekuwa ikigawa mashine ndogondogo kwa wananchi wa vijiji vya Wilaya ya Mkuranga ambako umeme bado haujafika ili kuwahamasisha kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Katika ziara hiyo, Bw. Nolasco Mlay pia alitembelea kampuni ya Matima Investment inayojishughulisha na utengenezaji wa majiko ya kuchomea nyama yanayotumia gesi, kwa lengo la kujionea namna majiko hayo yanavyosaidia kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.



Picha ya pamoja ya Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na Wadau wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kutoka Taasisi ya Wazalendo Movement Mkoani Pwani.

# JESHI LA MAGEREZA LATEKELEZA AGIZO LA SERIKALI LA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Gharama nafuu yawa chachu ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.
- Wizara ya Nishati yawapongeza



Kwenye picha ni namna Makaa ya Mawe yanavyoonekana ikiwa katika kutekeleza ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia Nchini.


Jeshi la Magereza nchini limetekeleza agizo la Serikali la matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 suala linaloifanya jeshi hilo kujikinga na athari zinazotokana na nishati isiyo safi ya kupikia kama vile kuni na mkaa.

Hayo yameelezwa na Kamishna Msaidizi wa Ofisi za Magereza Mkoani Simiyu Bw. Simon Kotti , wakati wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia walipofanya ziara kwa lengo la kufuatilia miradi ya usambazaji wa Nishati Safi ya Kupikia na Teknolojia zake ikiwemo matumizi ya Rafiki Briquettes katika Magereza ili kubaini changamoto mbalimbali kama zipo.

Kamishna msaidizi ameeleza kuwa kwa kuzingatia maelekezo ya agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia kwenye taasisi zinazolisha watu zaidi ya mia moja wao kama magereza walishalitekeleza hilo ili kujikinga na athari za matumizi ya nishati isiyo safi na salama.

Kotti amesema "sisi kama Jeshi la Magereza tunaendelea kuhakikisha tunajikita katika matumizi ya nishati safi ambapo kwasasa tunatumia nishati mbadala ya makaa ya mawe ambayo kulingana na uhitaji wetu tununua kwa gharama ya shilingi laki nane ikiwa ni gharama pungufu na kuni ambapo gharama yake ilikuwa mara mbili ya makaa ya mawe" amesema Kotti.

Sambamba na hilo Kamishna



Kwenye picha ni namna Makaa ya Mawe yanavyoonekana ikiwa katika kutekeleza ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia Nchini.

msaidizi wa Magereza Mkoani Simiyu amesema kwa upande wa Magereza ya Wilaya ya Bariadi inaendelea na mradi wa kujenga gesi vunde kwa ajili ya kupikia ambapo mradi huo upo katika hatua ya kukusanya vifaa vya ujenzi na utakapo kamilika utasaidia kuongeza chanzo kingine cha nishati safi na pia kuchangia katika utekelezaji wa Mkakati wa wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia.

Naye, Mtaalam kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Omari Khalifa amepongeza juhudi za Jeshi la Magereza nchini katika Utekelezaji wa agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia, huku akikisistiza umuhimu wa kuendelea kutumia nishati safi ili kujikinga na athari za kiafya na mabadiliko ya tabia nchi.

Aidha Bw. Khalifa ametoa angalizo la sehemu za kutunzia Mkaa wa Makaa ya mawe ili kuzuia athari zinazoweza kujitokeza endapo nishati hiyo haitotunzwa sehemu salama.

"Nasisitiza kuboresha sehemu za kutunzia Mkaa wa Makaa ya mawe, ili nishati hiyo isiweze kuathirika, kwani utunzaji mzuri utaendelea kusaidia kupata nishati iliyo bora zaidi na kwa kiwango kilichokusudiwa pasipo changamoto yoyote" amesema Bw. Khalifa.

Katika hatua nyingine Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati wametembelea Gereza la Musoma lililopo Wilaya ya Musoma Mkoani Mara ili kujionea miundombinu ya Nishati safi ya kupikia na jinsi nishati hizo zinavyotunzwa.



Kwenye picha ni namna shimo linavyoonekana ikiwa ni maandalizi ya uanzishaji mfumo wa Gesi vunde katika Gereza hilo.

# MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YAONGEZA UFANISI WA KAZI KWENYE MAGEREZA

- Mkuu wa Gereza Bukoba asema sasa Wafungwa hawaendi nje kutafuta nishati zisizo salama
- Nguvu kazi sasa inaelekezwa katika uzalishaji
- Mkurugenzi Nishati Safi ya Kupikia awapongeza: Ahamasisha ubunifu zaidi




Picha ya pamoja ya Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na Uongozi wa Jeshi la Magereza Bukoba katika ziara ya kuhakikisha agizo la matumizi ya nishati safi ya kupikia linatekelezwa.

Mkuu wa Gereza la Bukoba, Bw. Aloyce Kalihamwe amesema matumizi ya nishati safi ya kupikia yameleta mageuzi makubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Magereza nchini yakichangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi wa kazi, kulinda afya na mazingira pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa taasisi hiyo.

Akizungumza wakati wa ziara ya wataalam kutoka Wizara ya Nishati waliotembelea Gereza la Bukoba kufuatilia utekelezaji wa agizo la Serikali kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100, Bw. Kalihamwe amesema nishati safi ya kupikia imeondoa changamoto nyingi zilizokuwa zikiikabili taasisi hiyo hapo awali.

“NIishati safi ya kupikia pamoja na kulinda afya na mazingira, imekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha wafungwa hawaendi nje ya maeneo ya Gereza kutafuta nishati zisizo salama kama vile kuni, hali iliyokuwa ikihitaji ulinzi mkubwa na rasilimali nyingi.” Amesema

Ameongeza muda ambao ulikuwa ukitumika kwenda nje kulinda wafungwa kwa ajili ya utafutaji wa nishati isiyo safi ya kupikia pamoja na jitihada zilizokuwa zikitumika kuongeza ulinzi sasa zitatumika kufanya mambo mengine ya uzalishaji ndani ya Magereza.

Aidha ametanabaisha kuwa, matumizi ya nishati safi ya kupikia yamepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za ununuzi wa kuni pamoja na changamoto zilizokuwa



Mkuu wa Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Nolasco Mlay akilipongeza Jeshi la Magereza kwa kutekeleza kikamilifu agizo la Serikali la kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

zikijitokeza katika mchakato wa kuomba vibali vya ukataji miti kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Nolasco Mlay amelipongeza Jeshi la Magereza kwa kutekeleza kikamilifu agizo la Serikali la taasisi zote zinazolisha watu zaidi ya 100 kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Bw. Mlay amesema lengo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha afya na mazingira ya Watanzania yanaimarika kupitia matumizi ya nishati safi ya kupikia, akieleza kuwa hatua iliyochukuliwa na Jeshi la Magereza ni chachu ya kufikia lengo la Serikali la asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Aidha, Bw. Mlay amelishauri Jeshi la Magereza kuwa na zaidi ya chanzo kimoja cha nishati safi ya kupikia ili kuongeza ufanisi na uhakika wa matumizi ya nishati hiyo, sambamba na kuliasa Jeshi hilo kuendelea kuwa mfano na darasa kwa taasisi nyingine zinazolisha watu zaidi ya 100 nchini, ili zijifunze na kuhamasika kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia kama ilivyofanywa na Magereza yote 129 nchini.

Kwa upande mwingine, Mkurugenzi wa Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia ameahidi kulipatia Gereza la Bukoba majiko matatu ya kisasa yanayotumia nishati safi ya kupikia, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuimarisha miundombinu ya kisasa na rafiki kwa mazingira katika taasisi za umma.

# REA KULIONGEZEA UWEZO GEREZA LA KASULU KUZALISHA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Mashine ya kutengeneza mkaa mbadala kutolewa kuongeza nguvu ya uzalishaji nishati salama
- Ni hatua ya Serikali kuimarisha utekelezaji wa matumizi ya nishati safi katika taasisi



Mkuu wa Gereza la Kasulu, Bw. Vitalis Mkali, akielezea namna Gereza la Kasulu Mkoani Kigoma lilivyo tekeleza agizo la matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) italipelekea Gereza la Kasulu mkoani Kigoma mashine moja ya kisasa ya kutengeneza mkaa mbadala, hatua inayolenga kuliwezesha gereza hilo kuondokana na njia duni zilizokuwa zikitumika awali kuzalisha mkaa mbadala.

Akizungumza wakati wa ziara yake katika gereza hilo, Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Nolasco Mlay, amesema Serikali inaendelea kuunga mkono jitihada za taasisi mbalimbali nchini katika kuachana na nishati zisizo salama kwa kuwezesha upatikanaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira.

Amesema utoaji wa mashine hiyo utapunguza changamoto za upatikanaji wa mkaa mbadala kutoka maeneo ya mbali, kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuimarisha uzalishaji wa nishati safi kwa kutumia malighafi zinazopatikana kwa urahisi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Gereza la Kasulu, Bw. Vitalis Mkali, ameishukuru Serikali kwa hatua hiyo akisema mashine hiyo itasaidia kuzalisha mkaa mbadala wa kutosha, kuachana na mbinu duni za awali na kupunguza gharama zilizokuwa zikijitokeza wakati wa ununuzi wa nishati.

Amesema hatua hiyo itaongeza ufanisi wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ndani ya gereza sambamba na kulinda mazingira na kuboresha afya kwa watumiaji wa nishati hiyo.

Ziara ya Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia katika magereza mbalimbali ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Serikali la kuhakikisha taasisi zote zinazohudumia zaidi ya watu 100 nchini zinatumia nishati safi ya kupikia kama mkakati wa kulinda mazingira, kupunguza ukataji miti na kuboresha ustawi wa jamii.



Kwenye picha ni Wataalamu kutoka Wizara ya nishati pamoja na uongozi wa Gereza la Kasulu wakijionea namna mkaa mbadala unavyozalishwa Gerezani hapo.

# GEREZA LA KIBONDO LABUNI MKAA MBADALA KUTEKELEZA AGIZO LA SERIKALI LA NISHATI SAFI

- Ubunifu umelenga kulinda afya, mazingira na kupunguza gharama za matumizi ya nishati
- Wizara ya Nishati na TBS zapongeza; Zasisitiza viwango kuzingatiwa



Picha ya pamoja ya Wataalamu kutoka Wizara ya nishati pamoja na uongozi wa Gereza la Kibondo Mkoani Kigoma.

Jeshi la Magereza wilayani Kibondo mkoani Kigoma limeanza kutumia mkaa mbadala unaotokana na mchanganyiko wa maranda ya miti na udongo unaozalishwa ndani ya Gereza la Kibondo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Hayo yamebainika wakati wataalamu kutoka Wizara ya Nishati walipotembelea gereza hilo kwa lengo la kukagua na kujionea utekelezaji mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika taasisi za umma nchini.

Mkuu wa Gereza la Kibondo, Bw. Peter Shabani, amesema gereza hilo lilichukulia agizo la Serikali kama fursa ya ubunifu na kujitegemea kwa kutumia rasilimali zilizopo hatua ambayo inalenga kulinda afya, mazingira na kupunguza gharama za matumizi ya nishati

"Baada ya agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia, sisi kama Gereza la Kibondo tulilichukulia kama fursa. Kupitia wataalamu tulionao na kwa kushirikiana na wafungwa, tuliweza kubuni nishati yetu wenyewe kwa kutumia malighafi tulizonazo ili kupunguza gharama za kuagiza nishati kutoka nje." Amesema Bw. Shabani

Ameeleza kuwa mkaa huo mbadala umebuniwa na wafungwa waliopo gerezani hapo kama sehemu ya programu za urekebishaji tabia akibainisha kuwa kwa sasa nishati hiyo inatumika kwa matumizi ya ndani pekee kutokana na uhaba wa vifaa vya kisasa vya uzalishaji.

Kwa upande wake, Mtaalamu kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Bw. Masumbuko Noha, amepongeza hatua hiyo na kusisitiza umuhimu wa kufuata taratibu na viwango vya TBS endapo gereza hilo litaanza uzalishaji wa nishati hiyo kwa matumizi ya kibiashara.

"Ubunifu huu una tija kubwa, lakini ni muhimu kuhakikisha bidhaa hiyo inakidhi viwango vya ubora na usalama kabla ya kuanza kuuzwa kwa matumizi ya jamii," amesema Bw. Noha

Naye mtaalam kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Omary Khalifa, amesema ubunifu huo ni mfano mzuri wa utekelezaji wa sera ya nishati nchini, akilishauri Jeshi la Magereza Kibondo kuendeleza wazo hilo ili liwe fursa ya kiuchumi na chachu kwa taasisi nyingine.

"Hatua hii inaweza kuwa dira kwa taasisi nyingine nchini kuiga na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala, sambamba na kulinda mazingira na afya za wananchi," amesema Bw. Khalifa.

# GEREZA LA KILIMO URAMBO KUNEEMEKA NA MIUNDOMBINU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Mkuu wa Gereza Apongeza Juhudi za Serikali
- Asema Nguvu Kazi Sasa Inaelekezwa Kwenye Shughuli za Kiuchumi
- Ni Mwelekeo wa Serikali katika Kukidhi Mahitaji ya Umeme Ifikapo 2030




Kwenye picha ni Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati wakiwa pamoja na uongozi wa Gereza Urambo Mahabusu kwenye ziara ya kuangalia namna agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia lilivyotekelezwa.

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imepanga kupeleka majiko matatu ya kisasa yanayotumia mkaa mbadala pamoja na sufuria zake katika Gereza la Kilimo Urambo, mkoani Tabora.

Hatua hiyo ni sehemu ya jitihada za Serikali kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia katika taasisi zinazohudumia watu zaidi ya 100 nchini.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia, Bw. Nolasco Mlay, wakati wa ziara yake ya kikazi katika Gereza la Kilimo Urambo ambapo alijionea utekelezaji wa agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mlay amesema Serikali kupitia REA inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na kuziimarisha kwa miundombinu ya kisasa inayotumia teknolojia rafiki kwa mazingira kama majiko banifu na mifumo ya gesi.

Aidha, Bw. Mlay amesema Gereza la Mahabusu Urambo tayari limefungiwa mfumo mmoja wa gesi na kwa sasa linasubiri kupatiwa majiko manne ya gesi, Sambamba na hilo, gereza hilo pia litapatiwa majiko matatu yanayotumia mkaa mbadala ili kuendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia katika magereza nchini.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mkuu wa Gereza la Kilimo Urambo, Bw. Joseph Mzumara amepongeza juhudi za Serikali katika kuhakikisha taasisi na jamii kwa ujumla zinaachana na matumizi ya nishati zisizo salama kama kuni, ambazo zinaathiri afya na mazingira.

"Hapo awali tulikuwa


Kwenye Picha ni wataalamu kutoka Wizara ya nishati walipotembelea Gereza la Urambo Mahabusu Mkoani Tabora.

tunakabiliwa na changamoto kubwa za kutafuta kuni maeneo ya mbali, lakini kwa sasa tunatumia mkaa mbadala. Hali hii imesaidia kupunguza muda unaotumika kutafuta nishati zisizo salama na badala yake nguvu kazi inaelekezwa kwenye shughuli nyingine za kiuchumi," amesema Mzumara

Aidha, ameishukuru Wizara ya Nishati kupitia Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia kwa kuhakikisha nishati safi ya kupikia inawafikia pia watumishi wa Jeshi la Magereza.

"Watumishi wote tumepatiwa majiko ya gesi yanayotuwezesha kupika kwa haraka na kutekeleza majukumu yetu mengine kwa ufanisi zaidi badala ya kutumia muda mwingi kutafuta nishati zisizo salama," amesema.

Ameongeza kuwa Gereza la Kilimo Urambo lina mifugo ya kutosha, na kwa siku zijazo linajipanga kuanza kuzalisha gesi vunde (biogas) ili kujiongezea vyanzo endelevu vya nishati safi ya kupikia.


Kwenye picha ni mtungi wa gesi uliopelekwa Gereza la Urambo Mahabusu ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali la matumizi ya nishati safi ya kupikia.

# ELIMU YA NISHATI SAFI YATOLEWA KWA WATUMISHI MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA.

- Ni sehemu ya ushirikishwaji Taasisi za Umma katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia.
- Watumishi watakiwa kuwa Mabalozi wa kuhamasisha Nishati Safi ya Kupikia.



Elimu ya nishati safi ikitolewa kwa vitendo kwa Watumishi wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Katika jitihada za kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, Wizara ya Nishati kupitia kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia kimetoa mafunzo kwa watumishi 133 wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Akiwasilisha taarifa ya Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya nishati safi ya kupikia, Mhandisi Anitha Ringia kutoka Wizara ya Nishati ameeleza kuwa mafunzo hayo yamelenga kuongeza uelewa juu ya faida za nishati safi, ikiwemo kupunguza athari za kiafya na kimazingira zinazotokana na matumizi ya kuni na mkaa katika kupikia huku akiwaeleza Watumishi kuwa matumizi ya nishati safi ni sehemu ya ajenda ya kitaifa ya kulinda mazingira na kuboresha ustawi wa wananchi.

"Mafunzo haya yanaonesha dhamira ya Serikali katika kuhakikisha Taasisi za Umma zinakuwa mfano wa kuigwa katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na kupitia ninyi watumishi mtafanya uhamasishaji utakaoleta mwamko mpana zaidi kitaifa katika matumizi ya nishati safi na hatimaye kupunguza utegemezi wa nishati zisizo rafiki kwa mazingira." Amesema Ringia

Amesema Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha nishati safi inapatikana kwa urahisi, na inawanufaisha Watanzania wote ili kuhakikisha ifikapo 2034 asilimia 80% ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia.



Watumishi wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakipewa mafunzo ya matumizi ya nishati safi ya kupikia Jijini Dodoma.

Aidha Kupitia mafunzo hayo Mha. Ringia ametoa wito kwa watumishi wote wa umma kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia huku akiwahimiza kutumia uelewa walioupata kuwa mabalozi katika maeneo yao ya kazi na jamii wanazoishi.

Kwa upande wake Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Wizara ya Nishati Bi. Neema Mbuja ameeleza kuwa kupitia Mkakati wa Taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia wa Mwaka 2024 uliundwa Mkakati wa Kitaifa wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia lengo likiwa ni kuongeza uelewa wa umma na taasisi kuhusu umuhimu wa kutumia nishati safi ya kupika ili kufanikisha malengo ya Taifa ya kuhakikisha wananchi wanapika kwa kutumia nishati safi, salama na rafiki wa mazingira.

" Mkakati wa mawasiliano umetokana na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia na lengo lake ni kutoa elimu na kuwawezesha watanzania kupata taarifa sahihi juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, elimu hii wanaipata kupitia njia mbalimbali ikiwemo redio, televisheni, mitandao ya kijamii na maonyesho ya wazi, pia kupitia mkakati huu tumeendelea kuhamasisha umma na kufanya kampeni mbalimbali sambamba na kauli mbiu isemayo Nishati Safi ya Kupikia Okoa Maisha na Mazingira." Amesema Bi. Mbuja

Aidha Bi. Mbuja ameongezea kuwa Mkakati wa Mawasiliano umelenga kufikisha ujumbe kwa jamii kupitia vyombo vya habari, mikutano ya hadhara na mafunzo mbalimbali lakini pia kushirikisha kila mtanzania kulingana na rika na nafasi ya kila mtu mmojammoja kwa lengo la kuhakikisha ujumbe uliokusudiwa unawafikia Watanzania wote.

Naye Mhandisi Mwandamizi wa Utafiti kutoka Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO) Mha. Catherine Mwegoha ameeleza kuwa TANESCO imeendelea kutoa elimu juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia hususani nishati ya umeme kwani ni salama na nafuu kwa watumiaji hususani kwa kutumia majiko kama "Pressure Cooker" na "Induction cooker" (Jiko Janja ) kwani majiko haya yamefanyiwa utafiti na hupika vyakula vya asili kama vile ugali maharage makande na ndizi kwa kutumia umeme kidogo ukilinganisha na majiko mengine.

Akifunga Mafunzo hayo Mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - UTUMISHI ambaye ni Mkurugenzi wa uendelezaji Sera wa Ofisi hiyo Bw. Cyrus Kapinga amesisitiza kuwa ushiriki wao ni muhimu katika kuongeza kasi ya matumizi ya teknolojia bora na rafiki kwa mazingira kwa kuendelea kuchangia juhudi za Serikali katika kupunguza hewa ukaa na kulinda afya za wananchi.

"Sisi kama watumishi wa Umma ni sehemu ya jamii tunaopaswa kuhakikisha tunatekeza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati safi ya kupikia kwani kila Wizara ina jukumu la kuhakikisha watumishi wanatumia nishati safi hivyo katika kutekeleza hilo tutaanzisha mkakati wa ndani wa namna tutakavyopata majiko ya positive cooker kama Taasisi na kuhakikisha kila Mtumishi anapatiwa jiko hilo ili kila Mtumishi aweze kuendana na mabadiliko hayo."Amesisitiza Bw. Kapinga

Katika mafunzo hayo Watumishi walipata fursa ya kuona namna jiko janja (Induction Cooker) linavofanya kazi kwa ufaisi na kuokoa muda bila kutumia gharama kubwa.

# WADAU WAJADILIANA MBINU ZA KUFIKIA WALENGWA ILI KUFANIKISHA AJENDA YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Lengo ni kufikisha asilimia 80 ya watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034



Picha ya pamoja ya Wadau wa maswala ya nishati walipokutana Jijini Dodoma kujadili maswala mbalimbali yanayohusu nishati safi ya kupikia.

Wadau wa masuala ya Nishati safi ya kupikia zikiwepo Wizara na Taasisi mbalimbali nchini, wamekutana Jijini Dodoma na kujadili mbinu mbalimbali za kufikia wadau muhimu zitakazowezesha kufikisha asilimia 80 ya wananchi wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Mbinu zilizojadiliwa ni pamoja na upelekaji wa elimu ya Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia kwa Wananchi kupitia majukwaa na shughuli mbalimbali za Kijamii zikiwemo Mbio za Mwenge wa Huru pamoja na Siku ya mwanamke duniani, lengo likiwa kupitia kaulimbiu wananchi wanapata elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mhandisi kutoka Wizara ya Nishati Bi. Anita Ringia amesema kwamba "upo umuhimu wa ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wakiwemo vijana na watafiti ili kubuni suluhisho kupitia tafiti zao zinazoweza kusaidia kukuza maendeleo ya nishati safi ya kupikia badala ya tafiti hizo kuwekwa kabatini bila kutumika" amesema Ringia. Aliongeza kuwa litengenezwe jukwaa la kuwakutanisha watafiti na watekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia ili kupata suluhisho zinazohitajika kwa wakati sahihi" Amesema Ringia.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji kutoka Kampuni ya ushauri na usimamizi wa biashara (Kengo Limited), Bi. Sarah Majengo amesema lengo la kukutanisha wadau wa masuala ya Nishati safi ya kupikia ni kutambua wadau muhimu katika utekelezaji, majukumu yao, namna ya kuwafikia pamoja na kuendelea kukusanya maoni mbalimbali ambayo yatasaidia



Picha ya pamoja ya Wataalamu kutoka Wizara ya nishati walipokutana na wadau wa maswala ya nishati safi kupikia Jijini Dodoma.

kutekeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia sambamba na kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Wananchi.

"Matumizi ya nishati safi ya kupikia ni agenda mahususi ambayo imechukua nafasi kubwa katika Sera, Mipango na Mikakati ya Serikali, umuhimu wa agenda hii unasukumwa na ongezeko la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi" amesema Majengo.

Ameeleza kuwa, ushirikishwaji wa wadau utasaidia ujumbe wa nishati safi ya kupikia kufika kwa watu sahihi, kwa kuzingatia jinsia, majukumu ya kijamii pia utumiaji wa lugha ambayo inaeleweka kwa kila mwananchi.

# ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YATOLEWA KWA WATUMISHI WA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO.

- Watumishi watakiwa kuwa Mfano wa kuhamasisha Nishati Safi ya Kupikia.
- Waelezwa umuhimu wa mkakati wa mawasiliano kufikisha elimu ya nishati safi ya kupikia
- Katibu Mkuu apongeza



Mtalaamu kutoka Wizara ya Nishati akitoa mafunzo ya matumizi ya nishati ya kupikia kwa watumishi wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo katika Ofisi za Wizara hiyo, zilizopo Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

Wizara ya Nishati kupitia kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia kimetoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo katika Ofisi za Wizara hiyo, zilizopo Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma ambapo watumishi hao wameaswa kuwa mfano katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Mjiolojia Nsajigwa Mwambumbuli kutoka Wizara ya Nishati amewaeleza watumishi hao juu ya faida za nishati safi, ikiwemo kupunguza athari za kiafya na kimazingira zinazotokana na matumizi ya kuni na mkaa katika kupikia huku akiwaeleza Watumishi kuwa mfano wa kutumia na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Mafunzo haya ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini, hivyo dhamira ya Serikali ni kuhakikisha Taasisi za Umma zinakuwa mfano wa kuigwa katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na kupitia ninyi watumishi mtakuwa chachu ya mwamko mpana zaidi kitaifa katika matumizi ya nishati safi ya kupikia." Amesema Mwambumbuli

Ameeleza, Matumizi ya nishati isiyo safi imekuwa na athari kiafya, kiuchumi na kielimu ambapo amesema madhara hayo ni hatari kwa ustawi wa maendeleo katika jamii.

Kwa upande mwingine amesema kuwa Serikali na wadau kwa pamoja wanalenga kutimiza lengo la taifa la kuhakikisha nishati safi inapatikana kwa urahisi na inawanufaisha Watanzania wote ili kuhakikisha ifikapo 2034 asilimia 80% ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia.

Kwa upande wake Bw. Amanzi Kimonjo ambaye ni Afisa Habari kutoka Wizara ya Nishati ameeleza Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano unalenga kuongeza uelewa wa umma na taasisi kuhusu umuhimu wa kutumia nishati safi ya kupikia.

"Mkakati wa mawasiliano umetokana na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia na lengo lake ni kutoa elimu na kuwawezesha watanzania kupata taarifa sahihi na kwa urahisi juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, ambapo kutokana na maendeleo ya teknolojia habari ni rahisi kuwafikia wananchi kwa kutumia redio, televisheni, pamoja na mitandao ya kijamii ikiwa



Mtaalamu wa majiko ya umeme akitoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia

ni pamoja na twiter (x), thread, Instagram, Tik Tok, Facebook, na Youtube.

Aidha, ameongeza kuwa njia zingine za kufikisha elimu hiyo ni pamoja na kufanya kampeni mbalimbali za wazi ili kuwafikia wananchi kwa idadi kubwa

Naye Mhandisi Mwandamizi wa Utafiti kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Catherine Mwegoha ameeleza kuwa TANESCO imeendelea kutoa elimu juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia hususani nishati ya umeme kwani ni salama na nafuu kwa watumiaji hususani kwa kutumia majiko kama "Pressure Cooker" na "Induction cooker" (Jiko Janja ) kwani majiko haya yamefanyiwa utafiti na hupika vyakula vya asili kama vile ugali maharage makande na ndizi kwa kutumia umeme kidogo ukilinganisha na majiko mengine.

Akifunga Mafunzo hayo Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali Gerson Msigwa amesisitiza umuhimu wa watumishi wa wizara hiyo kuwa mabalozi wa matumizi ya nishati safi ya kupikia na kutoa pongezi kwa wawasilishaji kuhusu mada zilizowasilishwa.

"Watumishi wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo ni vyema kuwa mabalozi wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika makazi yetu na huu uelewa basi uendane na vitendo tunaporudi nyumbani tuwe wa kwanza kutumia nishati safi ya kupikia na kutoa elimu kwa wanajamii.

Katika mafunzo hayo Watumishi walipata fursa ya kuona namna jiko janja (Induction Cooker) linavyofanya kazi kwa ufaisi na kuokoa muda bila kutumia gharama kubwa.


Picha ya pamoja ya Wataalamu kutoka Wizara ya nishati walipokutana na wadau wa maswala ya nishati safi kupikia Jijini Dodoma.


For more info
www.nishati.go.tz